

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu:2460117  
Fax: 255 - 022 – 2460117  
e-mail: [info@psc.go.tz](mailto:info@psc.go.tz);  
[Secretary@psc.go.tz](mailto:Secretary@psc.go.tz);  
**Website:** [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
JENGO LA UBUNGO PLAZA,  
BARABARA YA MOROGORO,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

Tume ya Utumishi wa Umma inafanya Mkutano wake wa Kisheria Namba **1** katika mwaka wa fedha 2019/2020 ulioanza tarehe 19 Agosti, 2019 na unatarajiwa kumalizika tarehe 30 Agosti, 2019. Katika Mkutano huu Tume itapokea na kutolea uamuzi Rufaa na Malalamiko yaliyowasilishwa na Watumishi mbalimbali wa Umma, ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Waajiri na Mamlaka zao za Nidhamu.

Shughuli nyingine zilizopangwa kufanyika wakati wa Mkutano huu ni pamoja na kupokea na kujadili:-

- i) Taarifa ya ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

- ii) Taarifa ya ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha.
- iii) Taarifa ya ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.
- iv) Taarifa ya ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.
- v) Taarifa ya Ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA).
- vi) Taarifa ya ukaguzi maalum kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu uliofanyika katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) na;
- vii) Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume katika kipindi cha Robo ya Tatu (Januari hadi Machi, 2019) ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Tume inatekeleza majukumu haya kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Tume ya Utumishi wa Umma.  
**DAR ES SALAAM**  
20 Agosti, 2019